

Shule za Lugha ya Kifaransa

Milango Wazi kwa Wanafunzi Wapya

Sera mpya ya uchukuaji

Idadi ya watu wa Ontario's francophone imebadilika na tumejibu kwa miongozo mpya katika bodi za shule za lugha ya kifaransa. Bodi za shule zinabadili sera zao za uchukuaji na kuzifanya kuwa wazi zaidi na kuwa na mpangilio na kufanya shule za lugha ya kifaransa kuwa za kukaribisha zaidi.

Je! ni nani anaathiriwa na mabadiliko haya?

1. Wageni wazungumzao kifaransa
2. Wageni ambao hawazungumzi Kifaransa wala Kiingereza
3. Watoto ambao lugha ya kwanza ya akina babu zao ni Kifaransa.

Elimu ya lugha ya kifaransa na uingiaji katika Kifaransa

mu ya lugha ya kifaransa ni tofauti

Katika shule ya kifaransa, masomo yote katika mtaala wa Ontario hufunzwa kwa Kifaransa na shule zinatarajiwa kuhimiza 'kueleweka kwa utamaduni wa Kifaransa miongoni mwa wanafunzi. Uingiaji katika kifaransa ni kwa watoto ambao wangependa kujifunza lugha ya pili, katika shule ya umma au shule ya Kikatoliki inayofunza Kiingereza.

Jinsi ya kujiunga kwenye shule za lugha ya Kifaransa

Wazazi ambao wangependa kupeleka watoto wao katika shule zinazozungumza lugha ya Kifaransa lazima wawasilishe ombi kwa mkuu wa shule hiyo. Ikiwa mwanafunzi ni mtu mzima, yeye anaweza kuwasilisha ombi mwenyewe.

Kila bodi ya shule itakuwa na sera yake ya uchukuaji. Shule zitaweza kufafanua jinsi ya kuwasilisha ombi na ni hati zipi zinahitajika.

Hati za mwanafunzi

Hati zinazohitajika zinaweza kujumuisha:

- thibitisho la umri wa mwanafunzi
- thibitisho la mahali pa makazi pa mwanafunzi au mzazi
- rekodi ya masomo ya mwanafunzi
- rekodi ya chanjo ya mwanafunzi
- hati nyingine yoyote ambayo inaweza kusaidia katika kuchakata ombi, kama vile kidadisi cha kukusanya habari juu ya matumizi ya Kifaransa na lugha zinazozungumzwa na kuandikwa na wazazi.

Katika hali ambazo nyaraka zinazohitajika hazipatikani, shule inapaswa kutoa nyaraka mbadala. Katika hali kama hizo, bodi ya shule inaweza kuuliza wazazi au watu wazima kuthibitisha au kuitoa taarifa ilitoidhinishwa na thabiti inayotoa habari iliyombwa pamoja na kufafanua kwa nini nyaraka zinazohitajika hazipatikani.

Inapatikana katika lugha 8 kwenye www.edu.gov.on.ca/eng/amenagement/

English
English

Français
French

عربي
Arabic

Kreyol
Creole

Español
Spanish

Lingala
Lingala

Kiswahili

Tiếng Việt
Vietnamese

fikia kila mwanafunzi



Kigezo cha uchukuaji

Bodi za uchukuaji za shule zinapaswa kufafanua jinsi maombi ya mwanafunzi yanachakatwa na zinapaswa kujumuisha habari ifuatayo:

- kigezo, pamoja na kupima ambako kutatumiwa ikiwa mwanafunzi anaweza kuchukuliwa. Huku kunaweza jumuiisha:
 - kiwango cha mwanafunzi cha utaalum katika Kifaransa
 - kutaka kujua Kifaransa kwa mwanafunzi
 - kiwango cha matumizi ya Kifaransa na au kuwepo kwa utamaduni wa Kifaransa katika nyumba ya familia
 - umuhimu kwamba mzazi wa mwanafunzi anaambatisha lugha na utamaduni kwa jamii inayozungumza Kifaransa
 - kujitolea kwa mzazi kwa kusaidia kukua kwa mwanafunzi kielimu katika Kifaransa.
- madhumuni, yaliyomo na mpango wa mahojiano
- itachukua muda gani kwa kamati ya uchukuaji kuchakata ombi na kuamua
- kuna utawala kiasi gani katika kamati ya uchukuaji juu ya ikiwa kuchukua au kutochukua mwanafunzi.

Wazazi na wanafunzi watajifunza vipi kuhusu uamuzi wa shule?

Sera za uchukuaji zinapaswa kufafanua jinsi ambavyo maamuzi ya kamati yatawasilishwa.

- kamati inaweza kuambia wazazi ambao walituma ombi kuhusu uamuzi wake, lakini thibitisho liloandikwa lazima lifuatwe. Notisi ya uthibitisho inapaswa kuelezea misingi yoyote ya kukataliwa, ikiwa inatumika.
- kamati ya uchukuaji lazima iandike uamuzi wake na kuhakikisha kwamba hati inayohusiana inapatikana.

Baadhi ya bodi za shule zingependa kuweka mchakato wa kuhakiki maamuzi. Ikiwa hivyo, ni muhimu kwamba michakato ifafanuliwe wazi katika sera zao.

Jifunze zaidi kuhusu...

Elimu ya Lugha ya Kifaransa

Soma zaidi kuhusu elimu ya lugha ya Kiingereza huko Ontario katika kiungo hiki:

www.edu.gov.on.ca/eng/document/policy/linguistique/guide/index.html

Soma maelezo zaidi kuhusu sera zinaoongoza uchukuaji wa shule za Lugha ya Kifaransa katika kiungo hiki

www.edu.gov.on.ca/extra/eng/ppm/I48.html

Jinsi ya kupata shule au bodi za shule

Kitafuta Habari za Shule ni kifaa cha mtandaoni ambacho kinakuruhusu kutafuta shule yoyote inayofadhiliwa na umma na msimbo wa posta wa Ontario, mji/jiji, jina la shule au bodi ya shule. Unaweza pia kutafuta kwa kutumia anwani kutumia kichupo cha msimbo wa posta.

Ikiwa unatafuta shule ya lugha ya Kifaransa, utafutaji wa msimbo wa posta unapendekezwa.

www.ontario.ca/findschools

Tafuta bodi ya shule huko Ontario katika

www.edu.gov.on.ca/eng/sbinfo/

Maswali?

Kwa maelezo zaidi, tafadhali piga simu bila malipo kwenye 1-800-387-5514, au ikiwa unapiga kutoka Toronto piga kwenye 416-325-2929.